



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO



Tarehe: 21/04/2022

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro anawatangazia Wananchi wote ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro kuwa kuna nafasi wazi ya **Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira** ya Halmashauri ya Wilaya Ngorongoro kwa kipindi cha **miaka mitano**.

SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe Raia wa Tanzania na mwenye akili timamu, mstaafu katika Utumishi wa Umma mwenye umri wa kati ya miaka 55 hadi 65
- Awe mwadilifu,
- Awe na ujuzi na utaalamu katika moja ya fani zifuatazo:-
 - Menejimenti ya Rasilimali watu (Human Resource Management)
 - Utawala wa Umma (Public Administration)
 - Sheria (Law)

MALIPO

Kazi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira **haina mshahara**. Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira atalipwa posho ya vikao vya bodi kadiri vikao vitakapojitokeza au kadiri atakavyohudhuria vikao kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa na Serikali.

MAELEZO YA JUMLA

- Waombaji wote watume barua ya maombi zikiwa na viambatisho vifuatavyo:-
 - Cheti cha kuzaliwa
 - Nakala za vyeti vya elimu / Taaluma (Certified)
 - Barua ya utambulisho toka kwa mwenyekiti wa serikali ya kijiji ikiwa na picha ndogo tatu za hivi karibuni.
 - Wasifu binafsi (CV).
- Barua toka kwa wadhamini wawili (2) zikiwa na anuani kamili.
- Mwisho wa kupokea maombi ya kazi ni tarehe 04/05/2022 saa 9:30 Alasiri.
- Maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji (W)
Halmashauri ya Wilaya Ngorongoro,
S.L.P. 1,
LOLIONDO.

Tangazo limetolewa na:


Dkt. Jumaa Mohamed Mhina
**MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA
NGORONGORO**

